



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA**



**Kumb.Na. MZA/KDC/S.10/40/72**

**22 Juni, 2024**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba amepokea Kibali cha Ajira Mbadala kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupitia Barua yenye Kumb. Na. FA.228/613/01/C/028 ya tarehe 20 Juni, 2024. Hivyo, anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa za kujaza nafasi zifuatazo:

**1.0 MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III – NAFASI (4)**

**1.1 SIFA ZA KUAJIRIWA**

Waombaji wanatakiwa wawe wenye Elimu ya Kidato cha Nne (Form IV) au Sita (Form Six) aliyehitimu astashahada/cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**1.2 KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI**

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji mkuu wa serikali ya kijiji
- ii. Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika kijiji
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji wa mipango ya maendeleo ya kijiji
- iv. Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya kijiji;
- v. Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya kijiji;
- vi. Kutafsiri na Kusimamia Sera, Sheria na Taratibu;
- vii. Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali;
- viii. Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalama katika kijiji;
- ix. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji;
- x. Mwenyekiti wa kikao cha wataalam waliopo katika kijiji;
- xi. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi;
- xii. Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za kijiji; na
- xiii. Atawajibika kwa Mtendaji Mkuu wa Kata.

xiv. Pamoja na kazi nyingine utakazopangiwa na Mwajiri wake

### 1.3 MSHAHARA

Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali yaani **TGS B**.

### 2.0 MASHARTI YA JUMLA

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45 isipokuwa kwa wale tu walioko kazini Serikalini;
- ii. **Waombaji wawasilishe maelezo binafsi (Curriculum Vitae) yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye Anuani na Namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.**
- iii. Waombaji waambatanishe nakala za vyeti vya Kidato cha Nne au Sita, Taaluma na cheti cha kuzaliwa. Waombaji watakaowasilisha” Result Slip”,” Statement of Results”,” Provisional Results” au” Transcripts **HAVITAKUBALIKA.**
- iv. Kwa Waombaji waliosoma nje ya Nchi, Elimu ya Kidato cha Nne au Sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).
- v. Kwa waombaji waliosoma Vyuo nje ya Nchi wawasilishe uthibitisho kutoka Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).
- vi. Waombaji watakokidhi sifa zinazotakiwa ndio watakaoitwa katika usaili.
- vii. Barua ya maombi iliyosainiwa na Mwombaji inaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza au Kiswahili.
- viii. Waombaji wenye mahitaji maalum (special needs/disability) wanatakiwa kuainisha kwenye maombi yao.
- ix. Waombaji watakaowasilisha Taarifa za kughushi watachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria za Nchi.
- x. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi.
- xi. Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe **05 Julai, 2024**
- xii. Maombi yote yatumwe kwenye *mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo; <https://portal.ajira.go.tz/> (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa 'Recruitment Portal')*.

xiii. **Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili HAYATAFIKIRIWA.**

Tangazo hili limetolewa na;

**H.J MSANGA  
MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA KWIMBA.**

---

Mtaa wa Kakora, S.L.P 88, Ngudu, SIMU: +255 (028) 2983121, Nukushi: +255 (028) 2983119  
Barua Pepe: [ded@kwimba dc.go.tz](mailto:ded@kwimba dc.go.tz) , [dhro@kwimbadc.go.tz](mailto:dhro@kwimbadc.go.tz) , Tovuti: [www.kwimbadc.go.tz](http://www.kwimbadc.go.tz)

Uk. 3